

**RASIMU YA HOTUBA YA UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA
MAAFISA HABARI NA WATAALAM WA IT KWA MIKOA YA
KANDA YA ZIWA ILIYO TOLEWA NA KATIBU TAWALA WA
MKOA WA MWANZA C. P. CLODWIG MTWEVE KATIKA
UKUMBI WA VICTORIA PALACE HOTEL SIKU YA TAREHE 13
FEBRUARI, 2017.**

Mkurugenzi wa habari kutoka TAMISEMI,

Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka TAMISEMI

Mwakilishi kutoka PS3

Mwakilishi wa eGA

Wakufunzi wetu,

Waandishi wa habari

Ndugu washiriki, Mabibi na Mabwana.

Habari za Asubuhi.

Awali ya yote nimshukuru mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana hapa siku ya leo, hii imekuwa nafasi ya pekee ambapo wenzetu wa PS3 wametuwezesha sisi kukutana kwa ajili ya mafunzo haya ya siku nane, pili niwashukuru waandaji kwakunialika kuja kufungua mafunzo haya, kwani wangeweza kumualika mtu mwingine yeyote, nawashukuru sana kwa heshima hii mulonipa.

Ndugu wanasemina na waandaaji,

Nimeambiwa hii semina ya kwanza kabisa kufanyika hapa nchini, ambapo mara baada ya hapa, basi semina hii itaendelea kwenye maeneo mengine ya nchi, niwashukuru sana kwakuipa kipaumbele kanda hii ya ziwa inayo unganishwa na mikoa ya Mara, Kagera, Simiyu, Shinyanga na Mwanza ambayo ni mwenyeji, kwetu sisi Mwanza ni heshma ya kipekee hivyo

nawapongeza sana PS3 kwa kuichagua tena Mwanza kwa mara nyingine, tunasema karibuni sana.

Ndugu wanasemina na waandaaji,

Lengo la Semina hii, kwanza nikuwajengea uwezo Maafisa wa TEHEMA na Maafisa habari ambao kwa namna moja ninyi ndio mmekuwa wachakataji wa taarifa za serikali na kuhakikisha zinaufikia umma wa watanzania zikiwa katika hali ya ubora kwa kutumia njia mbali mbali za mawasiliano, kama vile mbao za matangazo na hata kwa njia ya mitandao.

Lakini katika kipindi chote hicho, ni ukweli kwamba, mmekuwa na changamoto ya namna gani mtafanya ili taarifa ziweze kutoka kwa wakati lakini pia utayarishaji wa Tovuti ambazo zitakuwa ni sehemu ya njia ya mawasilino kwa maana taarifa zote muhimu kuweza kuwekwa kwenye tovuti zenu za Mikoa na Halmashauri, niseme kuwa wenzetu wa PS3 wamekuja kutengua kitendawili.

Ndugu wanasemina na waandaaji,

Nimedokezwa kuwa mtakuwepo hapa Mwanza kwa siku nane, katika siku hizo nane, mtajifunza jinsi yakutengeneza Tovuti zitakazo saidia kuongeza ufanisi wa wakitangaza shughuli za serikali kwa uwazi na kupunguza kulalamikiwa katika utendaji wetu, lakini pia mafunzo haya yatawasaidia kufahamu njia mbadala za kujitangaza kwa umma na kutoa taarifa, sambamba na hilo itasaidia kuimarisha shughuli za utawala katika serikali na kufanya shughuli za serikali kufahamika kwa wadau wengine, mwisho mtasaidia uwepo wa taarifa sahihi za masuala ya bajeti na matumizi kwenye mikoa na Halmashauri zenu kupitia katika Tovuti zenu.

Ndugu wanasemina na waandaaji,

Nitoe rai yangu kwenu, katika siku zote mtakazo kuwepo katika semina, muitumie vizuri semina hii hasa ikizingatiwa kuwa, lengo la serikali ni kuongeza uwazi na wigo wa upatikanaji wa taarifa

sahihi naza uhakika za serikali katika tovuti ili kuiepusha serikali na habari za kuzusha na zisizo na maslahi kwa taifa, najua sio Halmashauri zote zenye Tovuti, lakini kupitia mafunzo haya mtakapo maliza wote mtakuwa tayari na Tovuti.

Ndugu wanasemina na waandaaji,

Niimani yangu baada ya hapa sasa, wananchi wataweza kuwapata kupitia mitandao ya kijamii na kufahamu shughuli mbali mbali zinazofanywa na mikoa yenu lakini pia Halmashauri zenu. Lakini pia ni fursa kwa wananchi kuweza kuuliza maswali na kujibiwa kupitia kurasa zenu za mitandao kwani hapo awali taarifa nyingi ziliwekwa kwenye mbao za matangazo na hazikutoa mwanya wa mwananchi kuuliza chochote.

Ndugu wanasemina nirudie tena kusema, Mwanza ni salama, basi kwa siku zote mtakazo kuwepo hapa msiache kutembelea sehemu mbali mbali ili mjionee mji wenu ambao unakuwa kwa kasi hivi sasa miongoni mwa miji iliyopo kusini mwa jangwa la Sahara lakini vile vile kuchangia uchumi kwa siku mbili tatu hizi msirudi makwenu bila kununua vijizawadi.

Mara baada yakusema hayo sasa, natamka rasmi kuwa, Semina ya siku Nane kwa Maafisa habari na Maafisa TEHAMA kwa mikoa ya Kanda ya ziwa imefunguliwa rasmi.

Mungu awabariki mwanzo hata mwisho wa Semina hii.

Asanteni kwakunisikiliza.

MWISHO